# RUANGWA DC

RUANGWA KWA MAENDELEO, IMEWEZEKANA TUNASONGA MBELE

Kitengo cha Mawasiliano Serikalini
Halmashauri ya Wilaya ya Ruangwa

JARIDA | Toleo Na. 04 | Oktoba, 2025 | www.ruangwadc.go.tz | @ruangwadc

HALIUZWI







ELIMU
AFYA
KILIMO, MIFUGO & UVUVI
TEHAMA
AJIRA
MIUNDOMBINU
MICHEZO
MAJI
NISHATI



Eng. Zuhura Rashid
DAS Ruangwa



Mhe. Hassan Ngoma
DC Ruangwa



Ndg. Frank Chonya
DED Ruangwa

# SAFU YA WACHANGIAJI

1. Nyambita Magoma
2. Aneth Kakiko
3. George Mganga
4. Daula Ally
5. Miraji Kessi



# Dibaji

Ni furaha kubwa kuwaletea wasomaji na wananchi wote wa Wilaya ya Ruangwa jarida hili la Halmashauri yetu, ambalo linakusudia kutoa taarifa sahihi, wazi na za kisera kuhusu hatua tunazopiga katika kuwaletea wananchi maendeleo endelevu. Jarida hili ni jukwaa muhimu la mawasiliano kati ya Serikali na wananchi, likionesha kwa uhalisia utekelezaji wa miradi, mafanikio, na jitihada mbalimbali zinazotekelezwa katika kila sekta ya huduma za jamii.

Halmashauri ya Wilaya ya Ruangwa imeendelea kuimarika katika nyanja zote Elimu, Afya, Miundombinu, Kilimo, Maji, na Nishati sambamba na kukuza mazingira rafiki ya uwekezaji. Mafanikio haya yanatokana na ushirikiano mzuri kati ya Serikali, wadau wa maendeleo, sekta binafsi, na wananchi wetu ambao wameendelea kuwa sehemu ya mabadiliko tunayoyashuhudia leo.

Tukiwa tumejipanga katika utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 na Ilani ya Chama cha Mapinduzi (CCM), Halmashauri inaendelea kuweka mkazo katika usimamizi wa rasilimali, uwazi katika matumizi ya fedha za umma, pamoja na kuimarisha uwajibikaji katika ngazi zote. Tumekuwa tukizingatia falsafa ya "Serikali kwa Wananchi" kwa kuhakikisha huduma zinawafikia wote bila ubaguzi, huku tukihamasisha ubunifu na matumizi ya teknolojia katika utoaji wa huduma.

Ninawashukuru sana viongozi wote wa ngazi mbalimbali, watumishi wa Halmashauri, wadau wa maendeleo, na wananchi kwa mchango wao mkubwa katika kutekeleza miradi na mipango tuliyojiwekea. Kila mafanikio tunayoyaona leo ni matokeo ya ushirikiano wenu na dhamira ya pamoja ya kuijenga Ruangwa yenye uchumi imara, wananchi wenye kipato bora, na huduma bora za kijamii.

Nawakaribisha wasomaji wote kufuatilia kurasa za jarida hili ili kushuhudia kwa kina matokeo ya kazi nzuri inayofanyika Ruangwa, tukiamini kuwa taarifa njema ni chachu ya hamasa, uwazi, na maendeleo endelevu.

***"Ruangwa kwa maendeleo, imewezekana tunasonga mbele."***



Ndg. Frank F. Chonya
Mkurugenzi Mtendaji
Halmashauri ya Wilaya ya Ruangwa




# MAENDELEO YA ELIMU YA AWALI NA MSINGI WILAYANI RUANGWA

*Na Aneth Kakiko, Ruangwa DC.*

Elimu ya awali na msingi ndiyo nguzo ya maendeleo ya kijamii, kiuchumi, kisayansi, kiteknolojia na kiutamaduni kwa taifa lolote. Halmashauri ya Wilaya ya Ruangwa imeendelea kuwekeza nguvu kubwa katika kuinua ubora wa elimu hiyo hususani katika kipindi cha uongozi wa Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan. Kupitia sera za elimu bure na utekelezaji wa miradi ya kitaifa ya kuboresha mazingira ya kujifunzia, watoto wengi sasa wanapata elimu bora katika mazingira rafiki na salama.




Wilaya ya Ruangwa ilikuwa ikikabiliwa na changamoto nyingi katika elimu ya awali na msingi. Shule nyingi zilikuwa na upungufu wa vyumba vya madarasa, vifaa vya kufundishia na walimu wa kutosha. Baadhi ya wanafunzi walilazimika kusoma chini ya miti au kushirikiana darasa moja kati ya madarasa mawili tofauti. Changamoto hizo zilichangia idadi ndogo ya watoto kujiunga na elimu ya awali na matokeo yasiyoridhisha katika elimu ya msingi.

Aidha Serikali ya awamu ya sita imeleta mabadiliko makubwa kwa kuimarisha bajeti ya elimu na kupeleka fedha moja kwa moja kupitia mifuko ya BOOST na EP4R ambayo imewezesha ujenzi wa shule mpya, ukarabati wa miundombinu na upanuzi wa vyumba vya madarasa. Idadi ya shule za msingi imeongezeka kutoka shule 86 mwaka 2020 hadi shule 98 mwaka 2025, shule 2 za mahitaji maalumu zilizoboreshwa na kujengewa nyumba 2 za walimu na mabweni 2 ya kisasa, shule 4 shikizi, huku kila shule ya msingi ikiwa na darasa la wanafunzi wa elimu ya awali. “Kupitia miradi ya BOOST Project na EP4R, tumefanikiwa kujenga na kukarabati shule nyingi, kupunguza msongamano wa wanafunzi darasani kutoka wanafunzi 90 mpaka 45, na kuboresha mazingira ya kujifunzia. Miradi hii imeleta mageuzi makubwa katika elimu ya awali na msingi hapa Ruangwa” haya yameelezwa na Afisa Elimu Awali na Msingi Wilaya ya Ruangwa Mwl. George Mbesigwe.

Miradi ya ujenzi wa madarasa mapya, ofisi za walimu, madawati na vyoo imekuwa ni kipaumbele cha Serikali ya awamu ya sita. Kwa kipindi cha miaka minne pekee, zaidi ya madarasa 48 kwa elimu ya awali yamekamilika, na shule nyingi zimepata miundombinu ya maji na vyoo bora. Hii imeondoa tatizo la msongamano wa wanafunzi darasani na kuboresha mazingira ya kujifunzia.

Kadhalika, Serikali imefanikiwa kuajiri walimu wapya wa shule za msingi na awali, ikiongeza idadi yao kutoka takribani walimu 478 mwaka 2020 hadi walimu 585 mwaka 2025.




Walimu wa elimu ya awali 7 wenye ujuzi na maarifa makubwa katika malezi ya watoto wadogo wameletwa mashuleni, huku mafunzo ya kitaaluma yakitolewa ili kuongeza ubunifu na mbinu bora za kufundisha watoto wadogo. Akizungumza na jarida hili, Mwl. Abdul

Nangomwa, Afisa Elimu Taaluma Msingi Wilaya ya Ruangwa amesema "Uwekezaji katika rasilimali watu mashuleni hasa walimu, viongozi na wataalamu wa elimu umeleta matokeo makubwa katika ubora wa elimu. Walimu waliopewa mafunzo, motisha na mazingira bora ya kazi wameongeza ubunifu na ufanisi katika ufundishaji. Wanafunzi sasa wanapata maarifa bora, ufaulu umeongezeka na nidhamu shuleni imeimarika hivyo tunawaandaa vizuri watoto wetu na kulijenga taifa lenye maarifa na ufanisi wa kiuchumi"




Matokeo ya uwekezaji huu yameonekana wazi katika ufaulu wa mitihani ya darasa la saba. Wastani wa ufaulu umeongezeka kutoka asilimia 87.1 sawa na wanafunzi 2666 walioandikishwa kufanya mtihani wa mwaka 2020 hadi asilimia 93 sawa na wanafunzi 3222 walioandikishwa kufanya mtihani wa mwaka 2024, huku idadi ya wanafunzi wanaojiunga kidato cha kwanza ikiongezeka kutoka wanafunzi 2000 mwaka 2020 mpaka wanafunzi 3085 waliojiunga mwaka 2025. Shule kama Likwachu, Likunja, Ruangwa na Chinongwe zimekuwa miongoni mwa shule zinazofanya vizuri kitaaluma katika mkoa wa Lindi.

Katika upande wa malezi ya watoto wa awali, Halmashauri imewekeza katika vifaa vya michezo, vitabu vya picha na programu za lishe shuleni. Shule zote zimenufaika na huduma za chakula cha mchana jambo linalowezesha watoto kuhudhuria kwa utaratibu na kuongeza umakini katika kujifunza. Mwalimu Jane Lugaka wa elimu ya awali amesema "Malezi bora kwa watoto wa awali ndiyo msingi wa mafanikio yao kielimu. Mtoto anapolelewa katika upendo, nidhamu na mazingira salama anakuwa na ujasiri na hamasa ya kujifunza".

Halikadharika, TEHAMA pia imeanza kuingizwa katika elimu ya msingi. Shule 15 ndani ya Wilaya zimepatiwa kompyuta na vifaa vya mafunzo ya kidigitali na walimu wote katika kila shule wamepatiwa vishikwambi. Walimu wamepewa mafunzo ya namna ya kutumia vifaa hivyo kufundisha masomo ya hisabati na kingereza, hatua inayokuza ubunifu na utayari wa wanafunzi kuingia katika elimu ya sekondari yenye mwelekeo wa kidigitali. Anna John mwanafunzi wa darasa la sita katika shule ya Ruangwa ameelezea namna TEHAMA inavyowasaidia katika masomo yao, "Tunapojifunza kwa kutumia kompyuta na television za elimu, tunafurahia masomo na kuelewa haraka. TEHAMA imetufanya tuwe wabunifu na tujifunze mambo mengi ya dunia bila kutoka darasani".

Kwa ujumla, mafanikio haya ni ishara ya utekelezaji mzuri wa dira ya Serikali ya awamu ya sita katika kuhakikisha kila mtoto anapata elimu bora kuanzia ngazi ya awali hadi msingi. Wilaya ya Ruangwa imepiga hatua kubwa katika kuboresha elimu na matokeo yake yanaonekana wazi kupitia ongezeko la ufaulu.








# MAPINDUZI KATIKA ELIMU YA SEKONDARI WILAYANI RUANGWA

*Na Aneth Kakiko, Ruangwa DC.*

Idara ya Elimu ya Sekondari katika Wilaya ya Ruangwa imeendelea kushuhudia mafanikio makubwa katika kipindi cha miaka minne chini ya uongozi wa Rais wa awamu ya sita Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, pamoja na usimamizi thabiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Ruangwa. Mabadiliko makubwa yamefanyika katika upatikanaji wa elimu bora, jumuishi na yenye tija.

Kabla ya mwaka 2021, Wilaya Ruangwa ilikuwa na jumla ya shule 20 za sekondari, zikiwemo chache zenye miundombinu hafifu na uhaba wa walimu, hasa katika masomo ya sayansi. Wanafunzi wengi walilazimika kutembea umbali wa zaidi ya kilomita10 kufika shuleni, hali iliyosababisha utoro na ufaulu duni. Kwa kipindi hicho, ufaulu wa kidato cha nne ulikuwa wastani wa asilimia 91, huku wanafunzi wachache wakiendelea na elimu ya kidato cha tano. Aidha, kupitia mpango wa elimu bure na ujenzi wa shule za sekondari kila kata, idadi ya shule imeongezeka kwa asilimia 95, hivyo kupunguza umbali wa wanafunzi kufuata elimu.

Ujenzi wa mabweni mapya 23, vyumba vya madarasa 48 na maabara 24 za sayansi, umefanyika kwa ushirikiano kati ya Serikali kuu, Halmashauri ya Wilaya, wadau wa maendeleo kwa pamoja na wananchi wa Ruangwa. Miongoni mwa shule zilizonufaika ni shule ya sekondari ya Ruangwa, Mandawa, Chinongwe, Narungombe na Mbekenyera ambazo sasa zina miundombinu inayokidhi mahitaji ya wanafunzi wote.

Kupitia miradi ya kuimarisha Elimu ya Sekondari (SEQUIP) na EP4R, shule zote zimepatiwa fedha za moja kwa moja kwa ajili ya ukarabati na ujenzi wa miundombinu. Fedha hizi zimetumika kujenga vyumba vya madarasa, ofisi za walimu, maktaba na vyoo vya kisasa, hivyo kuimarisha mazingira ya kujifunzia na kufundishia. Akiongea katika hafla ya kuwaaga kidato cha nne shule ya sekondari ya Chinongwe, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Ruangwa Ndg. Frank Chonya amesema "Maendeleo ya elimu ya sekondari Ruangwa ni matokeo ya usimamizi thabiti wa Serikali ya awamu ya sita. Tumeboresha miundo mbinu, tumeongeza ufaulu na tumeimarisha matumizi ya TEHAMA mashuleni. Halmashauri itaendelea kusimamia kwa karibu Idara ya Elimu ili kila mtoto wa Ruangwa apate elimu bora, salama na yenye tija kwa maendeleo ya taifa".

Katika kipindi cha uongozi wa Mhe. Dkt. Samia, Serikali imeongeza ajira za walimu wa sekondari kwa zaidi ya asilimia 70. Hadi sasa, Wilaya ina zaidi ya walimu 368 wa sekondari, ikilingashwa na walimu 247 waliokuwepo kabla ya mwaka 2021. Walimu hao wamepata mafunzo ya kuimarisha matumizi ya TEHAMA katika kufundisha. Akielezea mapinduzi ya TEHAMA, Mwl. Joel Mjema wa Mbekenyera Sekondari amesema "Siku hizi wanafunzi hawategemei vitabu pekee, bali wanajifunza kupitia kompyuta, vipaza sauti na mifumo ya kidigitali. Na sisi walimu tunatumia teknolojia kuandaa masomo, kuhifadhi taarifa na kufuatilia maendeleo ya wanafunzi kwa urahisi hivyo darasa limekuwa la kuvutia zaidi na imeongeza ubunifu kwa wanafunzi na maarifa mapana".

Uwekezaji katika Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) umeleta mapinduzi makubwa. Shule 4 zimejengewa madarasa mubashara yaliyounganishwa na televishioni janja, shule 14 zimepatiwa vifaa kompyuta na shule zote zinapata huduma ya intaneti. Walimu 25 wamepewa mafunzo ya matumizi ya teknolojia katika kufundisha, hatua inayosaidia wanafunzi kuwa na uelewa wa kisasa na kujiandaa kwa ushindani wa kidunia.

*Inaendelea ... Pg 22*




# WILAYA YA RUANGWA YAENDELEA KUNG'ARA KUPITIA MAPINDUZI YA KILIMO

*Na Nyambita Magoma, Ruangwa DC.*

Wilaya ya Ruangwa imepiga hatua kubwa katika sekta ya kilimo, ambapo eneo la mraba la 2,560 km² linafaa kwa matumizi ya kilimo, ekari 2,045 likifaa kwa mazao mbalimbali, huku wakulima zaidi ya 2,500 wakiendelea kunufaika na uwepo wa ghala la kisasa na linaendeshwa kwa mfumo wa stakabadhi ghalani.

Wilaya ilipokea matrekta matano, ikiwa ni sehemu ya mpango wa Serikali wa kusambaza zana za kilimo kwenye vituo 45 vya utoaji huduma nchini. Makabidhiano ya zana hizo yalishuhudiwa na Waziri Mkuu, Mhe. Kassim Majaliwa ambapo

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Ruangwa, ndugu Frank Chonya, alipokea matrekta hayo kutoka kwa Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Kilimo, Dkt. Hussein Mohamed Omary. Mpango huo unalenga kuboresha sekta ya kilimo kwa kuhakikisha wakulima wanapata nyenzo bora za kilimo ili kuongeza uzalishaji na tija.

Aidha, Mazao makuu yanayolimwa Ruangwa ni korosho, ufuta, mbaazi, mahindi, mihogo na alizeti, mazao ambayo yameendelea kuongeza kipato kwa kaya nyingi za wakulima. Pia Wilaya imeendelea kuwekeza katika kilimo cha ndizi, na ina eneo maalum la vitalu vya kuzalishia miche ya mazao mbalimbali ikiwemo korosho, parachichi, nazi na mazao mengine.




Hata hivyo, uwepo wa ghala bora la kisasa umeongeza tija ya kilimo, kuimarisha soko, na kuongeza kipato cha wakulima pamoja na familia zao. Mradi wa ujenzi wa ghala la mazao katika Kijiji cha Likangara, Kata ya Ruangwa, umejengwa kwa gharama ya shilingi bilioni 5,762,270,990.0, ukiwa na viwango vya kisasa vinavyowezesha kuhifadhi mazao kwa usalama huku likitumia mfumo wa stakabadhi ghalani.

Kadhalika, uwepo wa soko la pamoja limewezesha mazao kufika kwa wateja kwa urahisi, huku wanunuzi wakubwa wakiendelea kununua mazao kwa wingi, jambo linaloongeza mnyororo wa thamani ya mazao na kuondoa upotevu uliokuwa ukitokea hapo awali.

Vilevile, Serikali imewekeza katika kilimo kwa kutoa kwa ruzuku pembejeo za kisasa na mbegu bora huku ikiimarisha mifumo ya umwagiliaji katika maeneo mbalimbali ikiwemo Kata ya Nkowe na maeneo mengine ya Wilaya ya Ruangwa. Lakini pia, imeajiri maafisa Ugani kila Kata ili kuwasaidia wakulima kupata ushauri na ufuatiliaji wa karibu, huku ikihakikisha uwepo wa soko la uhakika la mazao.

Mbali na hayo, ujenzi wa barabara ya Ruangwa hadi Nanganga kwa kiwango cha lami, imekuwa chachu muhimu ya maendeleo ya kilimo kwa kurahisisha usafirishaji wa mazao na pembejeo kutoka mashambani hadi masokoni na maghalani, jambo lililopunguza gharama za usafiri na kuongeza ufanisi wa biashara za wakulima.



Akizungumza kuhusu manufaa ya ghala na mfumo wa stakabadhi ya ghala, Afisa Kilimo wa Wilaya, Nolasco Kilumile amesema, ghala la kisasa limekuwa msingi thabiti wa kuondoa upotevu wa mazao na kuongeza tija ya kilimo kwa wakulima wote wa Wilaya ya Ruangwa.

“Ghala na Mfumo wa stakabadhi ya ghala vimeleta uhakika kwa wakulima, wanauza mazao yao kwa bei nzuri na kuondoa upotevu, hii ni hatua kubwa kwa maendeleo ya kilimo Ruangwa.

Wakulima sasa wana uhakika wa soko na wanaweza kupanga mazao yao kwa njia ya kibiashara,” amesema Kilumile.

Naye, Meneja wa Ghala, Bi. Asha Ramadhani, akionesha jinsi ghala lilivyoimarisha biashara ya wakulima na kutoa huduma bora za kuhifadhi mazao, amesema: “Tumeboresha uhifadhi na uuzaji wa mazao kwa njia ya kisasa. Wakulima sasa wanapata malipo yao kwa uhakika na kwa muda muafaka. Mfumo wa stakabadhi ni jambo linaloongeza uaminifu wa soko na kurahisisha mauzo,” amesema Asha.

Kwa upande wake, Mkulima kutoka Kijiji cha Kitandi Bi. Rahma Hamisi, akizungumza kuhusu mafanikio makubwa ya sekta ya kilimo ikiwa ni pamoja na uhakika wa bei za mazao na uwepo wa ghala, zana bora za kilimo, soko la uhakika na wataalamu wa ugani kila Kata, amesema:

“Kwanza tulikuwa tukiuza mazao kwa bei ndogo na mara nyingi tulipoteza mazao kutokana na uhifadhi duni. Sasa kupitia vyama vya msingi na ghala letu kuu tunapata faida kubwa, mazao yetu yanahifadhiwa vizuri, na tunaweza kuuza kwa wakati unaofaa. Hii imesaidia familia zetu kifedha na kupanua biashara ndogo ndogo,” amesema Rahma.

Mbali na hayo, Sharifu Tepani, Mkazi wa Kata ya Mandawa ameishukuru Serikali kwa ruzuku ya pembejeo za kilimo na uboreshwaji wa bei za mazao ikiwa ni pamoja na zao la korosho ambalo kwa sasa limekuwa mkombozi wa maisha ya wanaruangwa.

“Ninamshukuru sana Rais Samia kwa kutujali sisi wakulima wa vijijini, kwa kweli katika suala la pembejeo Serikali imejitahidi sana. Tunajivunia namna tunavyopata pembejeo kwa wakati, na hata uzalishaji wa mazao umeongezeka sana kwa sababu hakuna mkulima anayeshindwa kununua viwatilifu, hata bei za mazao zinatufanya tupate moyo wa kulima kwa bidii” amesema Lifa.

Kwa ujumla, Wilaya ya Ruangwa inaonyesha maendeleo thabiti katika sekta ya kilimo, kutoka kwenye upatikanaji wa ghala la kisasa, uhifadhi bora wa mazao, stakabadhi ya ghala, soko la uhakika, na uwekezaji wa ndani na nje, hadi ongezeko la kipato cha wakulima na ajira kwa wanawake na vijana. Hali hii inaonesha jinsi kilimo kilivyokuwa msingi wa maendeleo ya jamii, ukuaji wa uchumi wa kijamii, na uwekezaji endelevu katika ya Wilaya ya Ruangwa.

















# ASILIMIA 85 YA WANANCHI RUANGWA WANUFAIKA NA MABORESHO YA HUDUMA ZA AFYA

*Na George Mganga, Ruangwa DC.*

Sekta ya afya katika Halmashauri ya Wilaya ya Ruangwa imepiga hatua kubwa katika kipindi cha hivi karibuni, hali iliyowezesha zaidi ya asilimia 85 ya wananchi kunufaika moja kwa moja na maboresho ya huduma za afya yaliyotekelezwa na Serikali pamoja na wadau mbalimbali wa maendeleo. Hatua hizi zimeleta ahueni kubwa kwa wakazi waliokuwa wakisafiri umbali mrefu kwenda kutafuta huduma za matibabu.

Kwa mujibu wa Mganga Mkuu wa Wilaya ya Ruangwa, Dkt. Feisal A. Said, ameeleza kuwa Wilaya kwa sasa inajivunia kuwa na vituo vya afya 10, zahanati 39 na Hospitali ya Wilaya moja ambayo imekuwa kitovu cha huduma kwa maelfu ya wananchi. Awali, Ruangwa ilikuwa na vituo vitatu pekee vya huduma za afya, hali iliyosababisha usumbufu mkubwa kwa wananchi hasa wa maeneo ya vijijini.

Aidha, Dkt. Feisal amesema kuwa kwa sasa ujenzi wa vituo vya afya vitatu unaendelea katika maeneo ya Nambilanje, Namakuku na Chinongwe, sambamba na ujenzi wa zahanati mbili katika vijiji vya Namilema na Lipande. Ujenzi huo unalenga kuongeza wigo wa upatikanaji wa huduma bora, kupunguza msongamano hospitalini na kuboresha huduma kwa wananchi vijijini.

Hospitali ya Wilaya ya Ruangwa imepata mafanikio makubwa kwa kuwekewa Power Plant ya kuzalisha hewa tiba (oxygen), hatua ambayo imeokoa maisha ya wagonjwa wengi hususan watoto wachanga na wagonjwa mahututi. Hewa hiyo inazalishwa ndani ya hospitali, hivyo kupunguza utegemezi wa hospitali za mbali kwa huduma hizo muhimu.

Hata hivyo, maendeleo hayo yamekwenda sambamba na uanzishaji wa Duka la Dawa la Jumla na Rejareja, ambalo limeongeza upatikanaji wa dawa kwa wagonjwa kwa wakati. Wagonjwa sasa hupata dawa ndani ya hospitali hiyo bila kulazimika kwenda kwenye maduka binafsi, hali ambayo imepunguza adha na gharama za matibabu.

Kwa upande wake, Dkt. Feisal amesema kuwa huduma za mama na mtoto zimeimari-









> **"Huduma za wajawazito na watoto wachanga sasa zinapatikana karibu na makazi ya wananchi, jambo lililowapa matumaini na amani ya moyo akinamama wengi, tofauti na ilivyokuwa awali,"** ***amesema Dkt. Feisal.***

ka kwa kiwango kikubwa, na hatua hiyo imechangia kupunguza vifo vya watoto wachanga na wajawazito. Huduma hizo sasa zinapatikana karibu na wananchi katika zahanati na vituo vya afya vilivyoboreshwa.

"Huduma za wajawazito na watoto wachanga sasa zinapatikana karibu na makazi ya wananchi, jambo lililowapa matumaini na amani ya moyo akinamama wengi, tofauti na ilivyokuwa awali," amesema Dkt. Feisal.

Baadhi ya wananchi wamepongeza maboresho hayo kwa kusema yameleta mabadiliko makubwa katika maisha yao. Bi. Asha Hamisi wa Chinongwe amesema, "Siku hizi tunapata huduma karibu kabisa na nyumbani. Mtoto akiumwa usiku, tunapata tiba mara moja bila hofu wala safari ndefu."



KITUO CHA AFYA MBUYUNI

Naye Bw. Juma Kitenge wa Namakuku amesema, "Huduma za upasuaji na uzazi zimekuwa mkombozi mkubwa. Zamani tulikuwa tukipeleka wagonjwa Ndanda, lakini sasa kila kitu kinapatikana hapa Ruangwa. Huu ni ushindi mkubwa kwa wananchi."

Kwa ujumla, mafanikio haya yameibadilisha sura ya sekta ya afya wilayani Ruangwa na kuonesha dhamira ya Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, ya kuboresha huduma za kijamii. Ruangwa sasa ni mfano halisi wa Wilaya inayotekeleza kwa vitendo sera ya maendeleo endelevu na ustawi wa wananchi wake.



# UJENZI WA BARABARA YA KILOMITA 53.2 NANGANGA - RUANGWA WABADILISHA MAISHA YA WANANCHI

*Na Miraji Kessi, Ruangwa DC.*

Wilaya ya Ruangwa imepiga hatua kubwa za kimaendeleo baada ya kukamilika kwa ujenzi wa barabara ya Nanganga–Ruangwa yenye urefu wa kilomita 53.2, uliogharimu zaidi ya shilingi bilioni 18 chini ya usimamizi wa Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA), hatua iliyorahisisha usafiri, kupunguza gharama na kuchochea shughuli za kiuchumi.

Kwa undani, barabara hii imekuwa mkombozi kwa wananchi wa Ruangwa na maeneo jirani. Kabla ya ujenzi wake, safari kutoka Nanganga hadi Ruangwa zilichukua zaidi ya saa tatu na nauli kufikia shilingi 10,000, lakini sasa safari hiyo huchukua saa moja na nusu pekee huku nauli ikishuka hadi shilingi 6,000. Wananchi wanasema mabadiliko hayo yameleta tija kubwa katika biashara, kilimo na upatikanaji wa huduma muhimu.

Kwa upande mwingine, Meneja wa TARURA Wilaya ya Ruangwa, Mhandisi Mashaka Nalupi, amesema barabara hiyo ni kiungo muhimu kati ya wilaya hiyo na mikoa jirani. "Kupungua kwa gharama na muda wa usafiri kumeongeza ufanisi katika biashara na upatikanaji wa huduma za kijamii," amesema Mhandisi Nalupi, akisisitiza kuwa TARURA inaendelea kuboresha barabara nyingine ndani ya wilaya hiyo.

Aidha, ujenzi huo umeleta matumaini makubwa kwa wakulima wa vijijini ambao sasa wanasafirisha mazao yao kwa urahisi sokoni. Bw. Bakari Mchopa, mkulima wa ufuta kutoka kijiji cha Nachingwea, amesema: "Hapo awali mazao yaliharibika njiani, lakini sasa kila kitu kinawahi na bei ni nzuri. Tunampongeza Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuleta maendeleo haya."

Vilevile, wafanyabiashara wamefaidika na miundombinu bora. Bi. Hawa Selemani, mfanyabiashara wa jumla mjini Ruangwa, amesema: "Usafiri si changamoto tena. Bidhaa kutoka Dar es Salaam zinawasili kwa wakati na wateja wanapata huduma bila usumbufu."

Kwa upande wa uongozi wa Wilaya, Mkuu wa Wilaya ya Ruangwa, Mheshimiwa Hassan Ngoma, amesema Serikali inaendelea kuboresha barabara za mitaa ili kuongeza ufanisi wa matumizi ya barabara kuu hiyo. "Barabara hii ni kichocheo cha maendeleo. Tunapanua maboresho hadi kwenye maeneo ya kilimo na biashara ili wananchi wote wanufaike," amesema Mhe. Ngoma.

Zaidi ya hayo, TARURA imeweka mikakati ya kuimarisha miundombinu ya barabara hiyo kwa kuongeza taa za barabarani, mifereji ya maji, na ukarabati wa kudumu. Mkurugenzi wa TARURA Mkoa wa Lindi amesema:

"Ruangwa ni mfano wa mafanikio ya uwekezaji katika miundombinu vijijini. Tunataka barabara hizi zidumu na ziwe salama mwaka mzima."

Kadhalika, Serikali kupitia Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imetangaza mpango mpya wa kujenga barabara ya Ruangwa Mjini hadi Namichiga yenye urefu wa kilomita 21 kwa kiwango cha lami kwa ufadhili wa Benki ya Dunia.

"Barabara za vijijini sasa zitakuwa na taa za barabarani ili wananchi wafanye kazi hata usiku. Tunamshukuru Rais Dkt. Samia kwa kuwezesha fedha hizi," amesema Waziri Mkuu.

Kwa kuongezea, Serikali inaendelea kuimarisha barabara za vijijini zisizo za lami kama vile Chikwale–Machang'.




# VETA RUANGWA YAFUNGUA MILANGO YA AJIRA KWA VIJANA

*Na Daula Ally, Ruangwa DC.*

Baadhi ya vijana 116 wilayani Ruangwa wamenufaika na mafunzo ya ufundi yanayotolewa na chuo cha VETA Nandagala hali inayowasaida kujiajiri na kuboresha maisha yao ya kila siku

Mafunzo yanayotolewa katika chuo cha VETA Nandagala yamekuwa mkombozi mkubwa kwa vijana wa ruangwa waliokua hawana ajira wala stadi za kazi. Kupitia kozi mbalimbali kama vile ufundi magari, umeme wa majumbani, ubunifu wa mavazi na ushonaji, uashi/ujenzi, ujasiriamali, matumizi ya kompyuta, utengenezaji wa sabuni, utengenezaji wa batiki na mapambo, vijana hao wameweza kupata maarifa ya vitendo. Kwa mujibu wa takwimu kutoka VETA, Zaidi ya vijana 311 wamefaidika tangu kuanzishwa kwa mafunzo hayo mwaka 2024-2025.

Aidha, baadhi ya vijana waliomaliza mafunzo hayo 81 wamehitimu katika kozi ya muda mrefu, 155 wamepatiwa mafunzo ya uanagenzi yanayofadhiliwa na ofisi ya Waziri Mkuu na vijana, 23 ni kutoka mazingira magumu waliopatiwa mafunzo kupitia mradi wa timiza malengo, 42 ni wanawake waliopata ujuzi wa ujasiriamali kupitia program maalum ya wanawake na samia.

Vilevile wanawake 145 wamejitokeza kwa wingi kushiriki mafunzo hayo, na kupatiwa ujuzi katika kozi za umeme, ufundi magari, ubunifu wa mavazi na ushonaji, mapambo, utengezaji wa sabuni na batiki hali ambayo imeongeza usawa wa kijinsia katika sekta ya ujuzi na kuashiria mwamko mkubwa wa wanawake kushiriki katika fani za kiufundi.

Kwa upande wake Mkuu wa chuo cha VETA Nandagala Selemani Mbaga amesema, "juhudi zinaendelea kufanyika ili kuboresha miundombinu na kuongeza walimu ili kukidhi mahitaji ya wanafunzi wanaoendelea kuongezeka na kuendeleza mpango wa kupanua wigo wa kozi kwa kufanya utafiti wa soko la ajira katika kuanzisha kozi kama vile uchimbaji wa madini, kilimo cha kisasa, ufundi bomba, uchomeleaji na upishi".

Mbali na hayo, Halmashauri ya Wilaya ya Ruangwa imekua mstari wa mbele kushirikiana na VETA kuhamasisha vijana kujiunga na mafunzo hayo kwa kupanua wigo wa vijana wanaopata mafunzo ya ufundi, kuwapatia vifaa na zana za kufundishia kwa ubia na wadau na pia kuboresha miundombinu ya kufundishia

Naye mmoja wa wahitimu wa kozi ya ushonaji na ubunifu wa mavazi Baraka Nawasa amesema, "baada ya kuhitimu nimeweza kujiajili kwa kununua mashine ya kushonea nguo na kutafuta fremu yangu binafsi hali ambayo imenifanya nisilale njaa na kusaidia kufundisha vijana wenzangu wa mtaani kwa ujuzi nilioupata kupitia VETA". Amesema Nawasa.

Kadhalika wazazi na walezi wameanza kuunga mkono juhudi hizo kwa kuwasihi watoto wao kujiunga na VETA badala ya kubaki mitaani bila shughuli maalum.

Kwa ujumla mafunzo ya VETA Nandagala yamekua chachu ya mabadiliko chanya kwa vijana wa Ruangwa kwa kuwapa ujuzi wa kujitegemea, kupunguza utegemezi na kuongeza fursa za kiuchumi katika jamii na kuhakikisha katika ukuaji wa uchumi na utekelezaji wa Dira ya Taifa na maendeleo.





# VIJIJI VYOTE 90 WILAYANI RUANGWA VYANUFAIKA NA NISHATI YA UMEME

***Na Nyambita Magoma, Ruangwa DC.***

Vijiji vyote 90 vya Wilaya ya Ruangwa sasa vimeunganishwa na umeme, hatua inayochochea maendeleo ya kijamii na kiuchumi, huku Kaya na biashara ndogo zikionekana kunufaika zaidi na huduma hiyo muhimu.

Mradi wa usambazaji umeme vijijini uliotekelezwa na Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) kwa ushirikiano na Serikali kupitia Wakala wa Nishati Vijijini (REA) umebadili sura ya maisha katika Wilaya ya Ruangwa, ambapo robo tatu ya vitongoji 435 tayari vina umeme. Kwa mujibu wa sensa ya mwaka 2022, Wilaya hiyo yenye wakazi 185,573 sasa ina zaidi ya nusu ya wananchi wanaotumia nishati hiyo kwa shughuli za uzalishaji, elimu, afya na biashara, hali inayoongeza kipato na ustawi wa jamii. Utekelezaji wa mradi huo mkubwa umeifanya Wilaya ya Ruangwa kuwa miongoni mwa Wilaya zilizounganishwa kikamilifu kwenye gridi ya Taifa, ikiwa na jumla ya Kaya 60,931 zenye wastani wa Watu 3 kwa kila kaya, na kwa mantiki hiyo, maelfu ya wakazi wa Ruangwa wananufaika moja kwa moja na huduma hii muhimu ya nishati.

Hata hivyo, Kupatikana kwa umeme kumeongeza kasi ya ukuaji wa biashara ndogo ndogo, kumewezesha ujenzi wa viwanda vidogo vya kusindika mazao ya kilimo, na kuboresha utoaji wa huduma za afya, elimu na TEHAMA. Aidha, shughuli kama useremala, uchomeleaji vyuma, ushonaji, uchakataji wa nafaka na uhifadhi wa samaki sasa zinafanyika kwa ufanisi zaidi kutokana na upatikanaji wa nishati ya uhakika, hali inayoinua kipato cha wananchi na kuchochea maendeleo ya uchumi wa Wilaya kwa ujumla.

Kwa upande wake, Meneja wa TANESCO Wilaya ya Ruangwa, Eng. Hassan Mustafa, amesema kuwa upatikanaji wa umeme katika vijiji vyote umeongeza kasi ya maendeleo, hasa katika sekta za biashara, elimu na afya.

“Tumehakikisha kila kijiji kinapata umeme ili wananchi waweze kuendesha shughuli zao za kiuchumi kwa ufanisi. Umeme sasa ni kichocheo cha maendeleo ya kweli Ruangwa,” amesema Bw. Mustapha.




Aidha, wajasiriamali wadogo wamekuwa miongoni mwa wanufaika wakubwa wa upatikanaji wa umeme. Mfanyabiashara wa chakula mjini Ruangwa, Bi. Hadija Mohamedi, amesema umeme umebadilisha mfumo wa kazi zake kwa kuongeza tija na kupunguza gharama.

“Zamani tulitumia majiko ya mkaa na mafuta ya taa, lakini sasa umeme umeturahisishia kazi na kupunguza gharama. Biashara zetu zinakuwa kwa haraka,” amesema Bi. Hadija.

Vilevile, sekta ya elimu nayo imenufaika, kwani shule nyingi zimeweza kutumia vifaa vya TEHAMA na vifaa vya kufundishia vya kisasa. Mwalimu Willium Shigoli wa Shule ya Msingi Likunja amesema umeme umeongeza ufanisi katika ufundishaji na kujifunza.

“Sasa tunatumia vya kielektroniki kuandaa maandalio ya masomo tunatekeleza majukumu kidjitali kwa sababu tuna nisharti ya kutosha vile vile, Wanafunzi wanajifunza kwa ufanisi na shule zimepata mwanga hata wakati wa usiku,” amesema Mwalimu Shigoli.

Kwa upande mwingine, huduma za afya zimeimarika kwa kiasi kikubwa kutokana na uwepo wa umeme katika zahanati na vituo vya afya. Dkt. Feisal Said, ambaye ni Mganga Mkuu Wilaya ya Ruangwa, amesema kuwa upatikanaji wa umeme umeokoa maisha ya wagonjwa wengi.

“Tulifika mahali tulikuwa tukihifadhi dawa kwa shida, huduma za upasuaji zilikiwa zikisuasua sana lakini sasa friji zinatumika ipasavyo, na huduma za usiku zimeboreshwa sana,” amesema Dkt. Feisal.

Zaidi ya hayo, Adelina Hamissi ambaye ni Mfanya biashara amesema, “biashara za ushonaji, saluni, gereji na ufundi umeme zimeongezeka katika vijiji vya Ruangwa. Wananchi wengi sasa wanajiajiri kwa kutumia nishati ya umeme kuendesha mashine ndogo za uzalishaji kama vile mashine za kusaga na kushona, hatua inayopunguza tatizo la ajira kwa vijana wetu. “Amesema.

Kwa mujibu wa takwimu, takribani asilimia 75 ya vitongoji vyote 435 vya Ruangwa vina umeme, jambo linalokadiriwa kunufaisha zaidi ya wananchi 120,000. Hii inamaanisha kuwa zaidi ya nusu ya wakazi wa Wilaya hiyo wanapata huduma ya umeme moja kwa moja, jambo ambalo linaimarisha ustawi wa kaya na kupunguza umaskini vijijini.

Mbali na manufaa ya kijamii, uwepo wa umeme umeongeza uwekezaji katika sekta mbalimbali ikiwemo kilimo, ambapo wakulima sasa wanatumia pampu za umeme kumwagilia mashamba yao, huku wengine wakianzisha viwanda vidogo vya kubangua korosho na kuchakata nafaka.

Kadhalika, upatikanaji wa umeme umeimarisha mawasiliano na matumizi ya teknolojia, kwani vituo vingi vya huduma za simu na intaneti sasa vinafanya kazi kwa ufanisi. Hii imerahisisha upatikanaji wa taarifa, huduma za kibenki na mawasiliano kati ya wananchi na taasisi mbalimbali.

Kwa upande wake, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Ruangwa, Ndugu Frank Fabian Chonya, amesema upatikanaji wa umeme katika vijiji vyote 90 ni ushahidi wa jitihada kubwa za Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan katika kuwaletea wananchi maendeleo. Ameishukuru Serikali kwa uwekezaji huo mkubwa pamoja na kumpongeza Mhe. Kassim Majaliwa, Mbunge Mstafu wa Jimbo la Ruangwa, kwa mchango wake mkubwa katika kufanikisha upatikanaji wa umeme huo.

“Tunamshukuru Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kuwekeza katika miundombinu ya nishati vijijini. Vilevile, tunatoa pongezi kwa Mhe. Kassim Majaliwa kwa juhudi zake za muda mrefu katika kuhakikisha kila kijiji kinapata umeme. Hii ni hatua kubwa katika safari ya maendeleo ya Ruangwa,” amesema Ndugu Chonya.

Aidha, Kijiji cha Mmawa kilichopo Kata ya Nandagala ndicho kijiji cha mwisho kuunganishwa na umeme, hatua iliyokamilisha rasmi mpango wa Serikali kuhakikisha vijiji vyote 90 vya Wilaya ya Ruangwa vinapata huduma hiyo muhimu. Wananchi wa kijiji hicho wamesema hatua hiyo imeleta furaha kubwa na matumaini mapya ya maendeleo, hasa katika sekta za biashara, elimu na huduma za jamii.

Kwa ujumla, mradi wa umeme katika vijiji vyote 90 umeleta mageuzi makubwa Ruangwa, ukitoa fursa kwa wananchi kuboresha maisha yao, kukuza uchumi wa vijiji na kuimarisha utoaji wa huduma za kijamii. Kwa sasa, umeme si tena huduma ya anasa bali ni nguzo ya maendeleo endelevu inayowasha matumaini mapya kwa wakazi wa Ruangwa.












# UWANJA WA MAJALIWA WACHOCHEA UCHUMI NA MAENDELEO YA MICHEZO RUANGWA

*Na George Mganga, Ruangwa DC.*

Ujenzi na uboreshaji wa Uwanja wa Majaliwa wilayani Ruangwa umefungua ukurasa mpya wa maendeleo ya michezo na uchumi katika Wilaya hiyo, ambapo sasa michezo imekuwa chanzo cha ajira, biashara na utalii wa ndani. Hatua hii ni matokeo ya uwekezaji mkubwa uliofanywa na Serikali ya Awamu ya Sita katika kuboresha miundombinu ya michezo nchini.

Kwa mujibu wa Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Sanaa, Michezo na Utamaduni wa Wilaya ya Ruangwa, Elias Ndamo, amesema uwanja huo umepata hadhi ya kitaifa kutokana na ubora wa nyasi zake, usalama wa wachezaji na nafasi kubwa ya watazamaji, hivyo kuruhusu mashindano ya Ligi Kuu ya Tanzania Bara kuchezwa huko. Uwanja huo umeifanya Ruangwa kuwa kituo kipya cha mashindano makubwa ya michezo kitaifa, na kuamsha ari ya vijana kushiriki katika michezo mbalimbali.

Aidha, Mhandisi wa Halmashauri ya Wilaya ya Ruangwa, Noel Kitundu, amesema kuwa maboresho zaidi yanaendelea kufanyika ili uwanja huo ukidhi viwango vya kimataifa. Maboresho hayo yanahusisha ujenzi wa majukwaa ya kisasa yanayo jengwa kwa vyuma hivyo kuufanya uwanja huo kuwa uwanja wenye hadhi ya kipekee nchini Tanzania, lakini pia, Halmashauri inamkakati wa kuufanya uwanja huo kuwa eneo la sports center kwa kujenga miundombinu ya kisasa na rafiki kwa mazingira ya michezo mbalimbali. Lengo ni kuhakikisha Uwanja wa Mjaliwa unakuwa miongoni mwa viwanja bora kabisa nchini.

Hata hivyo, mbali na Uwanja wa Mjaliwa, Halmashauri ya Wilaya ya Ruangwa pia inamiliki na kusimamia viwanja vingine kadhaa vya michezo katika maeneo mbalimbali, ikiwemo Uwanja wa Ruangwa veteran, uwanja wa Chinongwe, Uwanja wa Likunja na Uwanja wa Namichiga. Viwanja hivyo hutumika kwa mazoezi, ligi za Wilaya, na mashindano ya shule, hatua inayowajenga vijana kuibuliwa kimichezo mapema.

Kwa upande wake, Afisa Maendeleo ya Jamii wa Wilaya ya Ruangwa, Rashid Namkulala, amesema uwanja huo mkubwa umefungua fursa nyingi za kiuchumi kwa vijana na wanawake, kupitia biashara ndogondogo zinazofanyika wakati wa mechi na matukio ya michezo. Biashara za vinywaji, chakula, mavazi ya michezo na usafiri zimekuwa zikistawi kutokana na ongezeko la wageni wanaofika kushuhudia michezo.

"Uwanja wa Mjaliwa umeleta fursa nyingi za kipato. Vijana wanapata ajira katika usafi, ulinzi, uuzaji wa tiketi na biashara ndogo, wakati wanawake wananufaika kupitia mauzo ya vyakula na vinywaji. Haya ni mafanikio halisi kwa jamii yetu," amesema Namkulala.

Mbali na hilo, uwanja huo umechangia kwa kiasi kikubwa kukuza utalii wa michezo kwa kuvutia wageni kutoka Mikoa jirani kama Lindi, Mtwara na Ruvuma wanaofika kushuhudia michezo mikubwa. Ongezeko hilo la wageni limekuwa kichocheo cha mapato kwa Halmashauri kupitia kodi na huduma za malazi, chakula na usafiri.

Afisa Michezo wa Wilaya amesema kuwa dhamira ya Serikali ya Awamu ya Sita ni kuhakikisha Ruangwa inakuwa kitovu cha michezo katika Kanda ya Kusini. "Tumeweka msingi mzuri kupitia Uwanja wa Mjaliwa, lakini pia tunaboresha viwanja vya mitaa ili michezo iwe fursa ya kijamii na kiuchumi kwa wote," amesema.

Baadhi ya wananchi wameelezea furaha yao kutokana na maendeleo hayo. Bw. Rashid Mlinga wa Likunja amesema, "Zamani tulisikia michezo mikubwa ilikuwa ikifanyika mikoani, sasa tunashuhudia hapa kwetu. Vijana wetu wanapata nafasi ya kuonekana na kupata fursa ya kucheza kwenye ngazi za juu."

Kwa ujumla, Uwanja wa Majaliwa na viwanja vingine vya michezo wilayani Ruangwa vimekuwa chachu ya maendeleo.




# MRADI WA UFUGAJI SAMAKI WAINUA UCHUMI, LISHE ZA WANANCHI RUANGWA

*Na Miraji Kessi, Ruangwa DC.*

Sekta ya uvuvi wilayani Ruangwa imepata sura mpya baada ya kuanzishwa na kuboreshwa kwa miradi ya ufugaji wa samaki kwenye mabwawa, hatua inayowezesha wananchi kujipatia kipato, ajira na lishe bora, huku ikichochea maendeleo ya kiuchumi na kijamii.

Mradi wa kuboresha lishe unaofadhiliwa na IFAD na NORAD chini ya mpango wa AFDP, uliopo katika Kijiji cha Nahanga, Kata ya Mandawa, umeleta mageuzi makubwa katika maisha ya wananchi wa eneo hilo. Mradi huu unalenga kuongeza kipato kwa wanakikundi na kuboresha lishe kwa wananchi wa kata hiyo na Wilaya kwa ujumla.

Tayari wanakikundi 20 kutoka Kijiji cha Nahanga wamepatiwa mafunzo ya uchimbaji mabwawa, upandikizaji wa vifaranga, na ufugaji wa samaki kwa mbinu za kisasa. Kupitia ujuzi huo, wamewezeza kujitegemea na kuzalisha samaki wanaokidhi soko la ndani, huku wakiboresha lishe ya familia zao na jamii nzima.

Kwa undani zaidi, miradi hii ya mabwawa inatekelezwa kwa ushirikiano kati ya Serikali, vikundi vya vijana na wanawake, pamoja na wataalamu wa sekta ya uvuvi wanaotoa mafunzo ya kitaalamu kuhusu ufugaji bora wa samaki. Shughuli hizi zimeibadilisha Ruangwa kuwa kitovu kipya cha uvuvi wa mabwawa mkoani Lindi, ambapo vikundi mbalimbali vinajifunza elimu ya ufugaji wa samaki kutoka Nahanga.

Aidha, uzinduzi wa uwekaji wa vifaranga vya samaki katika Kijiji cha Nahanga, mnamo Oktoba 29, 2024 ulifanywa na Mkuu wa Wilaya ya Ruangwa, Mheshimiwa Hassan Ngoma, na kuhudhuriwa na viongozi wa Serikali, wataalamu wa uvuvi na wanavikundi wa eneo hilo.

Ambapo, jumla ya vifaranga 7,000 vya samaki aina ya Tilapia Sato waliwekwa kwenye mabwawa ya mfano, idadi iliyozidi lengo la awali la vifaranga 6,000, ikiwa ni mkakati wa kufidia upotevu wa asili unaoweza kujitokeza katika mazingira ya ufugaji. Samaki hao wamefugwa kwa kipindi cha miezi saba kabla ya kuvunwa.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Ruangwa, Bw. Frank Chonya, alieleza kuwa Halmashauri imejipanga kusimamia kikamilifu utekelezaji wa mradi huo.

“Mradi huu ni sehemu ya juhudi za Serikali kuhamasisha kilimo cha kisasa na uvuvi endelevu kwa manufaa ya jamii. Halmashauri tuna dhamira ya kuendeleza mradi huu kwa kutoa ushirikiano zaidi,” amesema Ndg. Chonya.

Kwa upande wake, Afisa Kilimo wa Wilaya, Bw. Nolasco Kilumile, amesema kuwa Halmashauri ilipokea shilingi milioni 128 kwa ajili ya ujenzi wa shamba darasa la ufugaji wa viumbe maji, na kuongeza milioni 23.3 kumalizia miundombinu ya ofisi, vyoo na mashimo ya maji taka.

“Fedha hizi zimechangia ujenzi wa mabwawa ya mfano, ambayo sasa ni sehemu ya mafunzo kwa wanavikundi na shule za sekondari zinazofundisha kilimo cha uvuvi,” alisema Bw. Kilumile.

Naye, Afisa Uvuvi wa Wilaya ya Ruangwa, Bw. Hassani Mdoembazi, amewasisitizia wanavikundi kuzingatia mafunzo ya kitaalamu wanayopewa.

“Ni muhimu kufuata miongozo yote ya kitaalamu. Tukifanya hivyo kwa umakini, mradi huu utafanikiwa



kwa asilimia mia moja," alisema Bw. Mdoembazi.

Mradi huu umewezesha pia mafunzo kwa vikundi vitano vingine katika vijiji vya Chikoko, Chinokole, Michenganyumba, Namahema, na Nandagala, ambako shughuli za uchimbaji mabwawa zipo katika hatua za mwisho kabla ya kupatiwa vifaranga na chakula cha samaki.

Zaidi ya hayo, miradi huu umekuwa kichocheo cha ajira hasa kwa vijana, ambapo baadhi yao sasa wanajikita katika kazi za uvunaji, usindikaji na usambazaji wa samaki sokoni. Wengine wameanzisha biashara ndogo ndogo zinazohusiana na sekta hiyo, ikiwemo uuzaji wa chakula cha samaki.

Kadhalika, mabwawa haya yamechangia kuboresha lishe ya wananchi. Familia nyingi sasa zinapata samaki kwa urahisi, jambo linalosaidia kupunguza tatizo la utapiamlo, hasa kwa watoto. Wananchi wanasema samaki wanaozalishwa Ruangwa ni wa ubora wa hali ya juu na wanauzwa hata nje ya Wilaya. Kwa ujumla, uvuvi wa mabwawa umeibuka kuwa nguzo muhimu ya uchumi wa ndani Ruangwa. Mradi huu si tu unaongeza kipato cha wananchi, bali pia unakuza umoja wa kijamii, unaleta fursa za ajira, na kuchochea ustawi wa familia. Kwa ujumla, sekta ya uvuvi sasa ni injini mpya ya maendeleo wilayani Ruangwa, ikiweka msingi thabiti wa uchumi endelevu kwa kizazi cha sasa na vizazi vijavyo.





**Mradi huu ni sehemu ya juhudi za Serikali kuhamasisha kilimo cha kisasa na uvuvi endelevu kwa manufaa ya jamii. Halmashauri tuna dhamira ya kuendeleza mradi huu kwa kutoa ushirikiano zaidi - amesema Ndg. Chonya.**






# MAENDELEO MAKUBWA YA SEKTA YA MAJI RUANGWA YABADILISHA MAISHA YA WANANCHI

*Na Nyambita Magoma, Ruangwa DC*

Wilaya ya Ruangwa imepiga hatua kubwa katika upatikanaji wa huduma ya maji safi na salama kufuatia uwekezaji mkubwa wa Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, ambaye ameruhusu fedha nyingi kutekeleza miradi ya maji yenye thamani ya zaidi ya shilingi bilioni 184. Hatua hiyo imewezesha huduma ya maji kufika katika vijiji zaidi ya 55, ikiwemo mji mdogo wa Nyangao hadi Ruangwa.

Kwa mujibu wa Wizara ya Maji kupitia Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA), mradi mkubwa wa maji wa Nyangao – Ruangwa – Nachingwea umeanza kutekelezwa kwa lengo la kufikia azma ya kitaifa ya kuhakikisha wananchi vijijini wanapata huduma ya maji safi kwa zaidi ya asilimia 85. Mradi huo unahusisha vijiji 34 vya Wilaya ya Ruangwa, vijiji 21 vya Wilaya ya Nachingwea na kijiji kimoja cha Wilaya ya Lindi, ukihudumia jumla ya wakazi wapatao 128,657.

Aidha, chanzo cha maji cha mradi huo kina uwezo wa kuzalisha wastani wa lita milioni 15 kwa siku, wakati mahitaji kwa vijiji vinavyonufaika kwa kipindi cha miaka 20 ijayo yanakadiriwa kuwa lita milioni 6.9 kwa siku. Hivyo, kiwango hicho cha uzalishaji kimepangwa kuhimili ongezeko la watu na maendeleo ya miji katika kipindi cha muda mrefu.

Vilevile, Mkuu wa Wilaya ya Ruangwa, Mhe. Hassan Ngoma, amesema miradi hiyo ni matokeo ya maono ya Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan katika kuhakikisha wananchi wa vijijini hawapati tena shida ya maji. Akifafanua, Mhe. Ngoma alisema:

“Rais Dkt. Samia ameidhinisha zaidi ya shilingi bilioni 4.577 kwa miradi ya maji ndani ya Ruangwa pekee, na shilingi bilioni 119.1 kwa mradi mkubwa unaotoka Lindi kwenda Ruangwa hadi Nachingwea. Jukumu langu ni kusimamia ubora wa miradi hii ili idumu vizazi na vizazi na kumtua mama ndoo kichwani.”

Sambamba na hilo, Serikali inatekeleza mradi mwingine wa maji katika kijiji cha Nchimbila B wilayani Ruangwa utakaowanufaisha wakazi wa vijiji kadhaa. Mradi huo unagharimu takribani shilingi bilioni 119 na unatarajiwa kuongeza upatikanaji wa maji safi kwa wakazi wengi zaidi wa wilaya hiyo.

Kwa upande mwingine, Serikali kupitia mpango wa uchimbaji wa visima vitano vya maji safi na salama imeendelea kupunguza changamoto ya upatikanaji wa huduma hiyo. Mradi huo wenye thamani ya shilingi milioni 325 unatekelezwa chini ya usimamizi wa RUWASA, ukiwa ni sehemu ya utekelezaji wa agizo la kitaifa la kila Mbunge kuchimba visima vitano jimboni kwake ili kufikia maeneo yaliyokuwa hayana huduma ya maji kabisa.

Hata hivyo, Kaimu Meneja wa RUWASA Wilaya ya Ruangwa, Mhandisi Moshi Ngote, amesema miradi hiyo inatekelezwa kwa kuzingatia ubora na viwango vya kitaalamu vya ujenzi wa miundombinu ya maji. Akisisitiza hilo, Eng. Ngote alisema:

“RUWASA imejipanga kuhakikisha kila mradi wa maji unaotekelezwa Ruangwa unakidhi vigezo vya ubora, unahudumia wananchi kwa muda mrefu, na unakuwa endelevu kwa miaka mingi ijayo.”

Kwa upande wake, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Ruangwa, Ndugu Frank Chonya, amepongeza Serikali ya Awamu ya Sita kwa namna inavyowekeza katika sekta




ya maji. Akizungumza kuhusu hilo, alisema:
"Tunaishukuru sana Serikali ya Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kutuletea miradi mikubwa ya maji. Miradi hii inabadilisha maisha ya wananchi na kuongeza tija katika sekta nyingine kama afya, elimu na uchumi wa kaya."
Zaidi ya hayo, wananchi wa maeneo yanayonufaika wameonyesha furaha kubwa kutokana na kupatikana kwa huduma ya maji safi karibu na makazi yao. Akizungumza kwa niaba ya wananchi, Bi. Mwanaheri Bakari amesema: "Kwa kweli Serikali imefanya kazi kubwa sana. Kabla ya miradi hii tulikuwa tukitembea umbali mrefu kutafuta maji, lakini sasa maji yapo karibu na nyumba zetu. Tunamshukuru Rais wetu Mama Samia kwa kutuondolea adha hii."
Miradi ya maji inayotekelezwa Ruangwa imekuwa chachu ya maendeleo ya kijamii na kiuchumi. Wananchi wameanza kutumia muda zaidi katika shughuli za uzalishaji badala ya kutafuta maji, afya za jamii zimeimarika, na wanawake pamoja na watoto wameondokana na adha ya kubeba ndoo vichwani kwa umbali mrefu.
Kwa ujumla, sekta ya maji Ruangwa imeendelea kuwa mfano wa mafanikio ya sera za Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan. Uwekezaji mkubwa uliofanyika umejenga matumaini mapya kwa wananchi wa Ruangwa, ukiweka msingi imara wa maendeleo endelevu na ustawi wa jamii kwa kizazi cha sasa na vizazi vijavyo.

**"Mhe. Rais Dkt. Samia ameidhinisha zaidi ya shilingi bilioni 4.577 kwa miradi ya maji ndani ya Ruangwa pekee, na shilingi bilioni 119.1 kwa mradi mkubwa unaotoka Lindi kwenda Ruangwa hadi Nachingwea. Jukumu langu ni kusimamia ubora wa miradi hii ili idumu vizazi na vizazi na kumtua mama ndoo kichwani."** ***amesema Mhe. Ngoma***




**SIKILIZA 88.4**

**RUANGWA FM**




# TEHAMA YABADILISHA SURA YA MAENDELEO RUANGWA

*Na Daula Ally, Ruangwa DC*

Maendeleo ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) yamekuwa injini mpya ya mageuzi ya kiutendaji, kiuchumi na kijamii katika Wilaya ya Ruangwa, yakirahisisha utoaji wa huduma, ukusanyaji wa mapato na usimamizi wa rasilimali kwa uwazi na ufanisi mkubwa.

Katika wilaya yenye kata 22, vijiji 90 na vitongoji 435, inayokaliwa na wakazi wapatao 185,753, matumizi ya mifumo ya kidijitali yameleta mapinduzi makubwa katika namna wananchi wanavyopata huduma za serikali, taarifa za afya, leseni za biashara, na huduma za kifedha kwa urahisi na kwa muda mfupi zaidi.

Kwa mujibu wa taarifa kutoka Kitengo cha TEHAMA cha Halmashauri ya Wilaya ya Ruangwa, zaidi ya asilimia 75 ya wananchi sasa wanatumia huduma za kidijitali katika shughuli zao za kila siku, hatua inayothibitisha kasi kubwa ya mabadiliko ya kiufanisi wilayani humo.

Aidha, kupitia mfumo wa TAUSI Portal, wananchi wa Ruangwa sasa wanaweza kupata leseni za biashara, vibali vya ujenzi na huduma nyingine za Halmashauri kwa njia ya mtandao bila kulazimika kufika ofisini. Mfumo huu umepunguza gharama za usafiri, muda wa kupata huduma, na umeongeza uwazi katika utoaji wa huduma za Serikali.

Vilevile, zaidi ya asilimia 60 ya wajasiriamali wadogo wilayani humo wanasajili biashara zao na kupata leseni kupitia TAUSI Portal. Hatua hii imeongeza mapato ya ndani na kupunguza mianya ya upotevu wa fedha kwa kubadili mfumo wa malipo kuwa wa kielektroniki kupitia POS Machine.

Zaidi ya hayo, kwa mujibu wa takwimu za Halmashauri, ukusanyaji wa mapato ya ndani umeongezeka kwa zaidi ya asilimia 30 ndani ya kipindi cha miaka miwili, hali inayoonesha namna teknolojia inavyoongeza tija katika usimamizi wa rasilimali.

Kadhalika, kupitia Watumishi Portal, watumishi wa umma sasa wanapata taarifa zao za mishahara, likizo, na taarifa za kiutumishi kwa urahisi zaidi. Mfumo huu umepunguza muda wa kushughulikia maombi mbalimbali kutoka wastani wa siku 14 hadi chini ya siku 5, huku ukiboresha mawasiliano kati ya Halmashauri na watumishi wake.

Hata hivyo, sekta ya afya imepiga hatua kubwa kupitia mfumo wa GoT-HoMIS uliosimikwa katika vituo vya afya vyote, hospitali ya wilaya na baadhi ya zahanati. Mfumo huu unadhibiti taarifa za wagonjwa, dawa, maabara, kliniki na malipo kwa njia ya kielektroniki — hatua inayowezesha huduma bora na takwimu sahihi za afya.

Afisa TEHAMA wa Halmashauri, Bw. Ramadhani Zombe, amesema:

"Kupitia mfumo wa GoT-HoMIS, muda wa kusubiri huduma umepungua kwa zaidi ya asilimia 50. Taarifa zote za wagonjwa zinapatikana kwa haraka, jambo lililoboresha huduma kwa wananchi na kupunguza foleni katika vituo vya afya."

Sambamba na hayo, Halmashauri ya Wilaya ya Ruangwa imepiga hatua kubwa katika eneo la manunuzi ya umma kwa kutumia mfumo wa NeST (National e-Procurement System of Tanzania), mfumo wa kitaifa wa manunuzi ya kielektroniki unaosimamiwa na PPRA.

Kupitia mfumo huu, zabuni zote, michakato ya manunuzi, na malipo kwa wazabuni hufanyika kwa uwazi na ufuatiliaji wa moja kwa moja. Hatua hii imepunguza urasimu, imeondoa mianya ya upotevu wa fedha za umma, na kuongeza uwajibikaji wa watendaji.

Kwa mujibu wa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Ruangwa, Ndugu Frank

Chonya, amesema:
"Kupitia NeST, taratibu zote za manunuzi sasa zinafanyika kwa uwazi wa kidijitali. Halmashauri inafuata kikamilifu Sheria ya Manunuzi ya Umma na mifumo yote inachangia kuongeza thamani ya fedha za wananchi. Mwaka 2024/2025, Halmashauri yetu imeshika nafasi ya nne kitaifa katika matumizi ya NeST na tulipata tuzo."




Kwa upande mwingine, upanuzi wa huduma za intaneti za hotspot katika maeneo ya ofisi za umma, shule, hospitali, na masoko umewezesha wananchi kupata taarifa na huduma kwa urahisi zaidi. Huduma hizo zimeongeza ushiriki wa wananchi katika shughuli za kiserikali, kielimu na kijamii kwa njia za mtandaoni.

Kwa mujibu wa takwimu za Halmashauri, upatikanaji wa huduma za intaneti umeongezeka kutoka asilimia 40 mwaka 2022 hadi asilimia 82 mwaka 2025 — hatua inayochochea elimu ya kidijitali, ubunifu na tija kwa vijana.

Kwa ujumla, matumizi ya TEHAMA yameleta mapinduzi makubwa wilayani Ruangwa. Wananchi wanapata huduma kwa wakati, serikali inakusanya mapato kwa uwazi, taarifa zinahifadhiwa salama,




na huduma za kijamii zinawafikia watu wengi zaidi.

Kwa maana rahisi, TEHAMA imekuwa injini ya mageuzi ya maendeleo Ruangwa, ikiimarisha utawala bora, uwazi, na ufanisi katika utoaji wa huduma kwa wananchi.






# WILAYA YA RUANGWA IMEBARIKIWA ARDHI YENYE HAZINA YA MADINI YA THAMANI

*Na Nyambita Magoma,*
*Ruangwa DC*

Wilaya ya Ruangwa imeendelea kuonesha dira ya maendeleo kupitia sekta ya madini, sekta ambayo imekuwa kichocheo kikuu cha uchumi wa ndani na chanzo cha ajira kwa wananchi. Eneo hili limebarikiwa kwa madini adimu yenye thamani ya kimkakati duniani, yakiwemo graphite, dhahabu, shaba, chuma, pamoja na madini ya vito kama Red Garnet na Green Garnet, yanayopatikana katika maeneo mbalimbali ya Wilaya.

Moja ya miradi mikubwa inayotoa mchango mkubwa katika sekta ya madini Ruangwa ni Mgodi wa Namungo, unaojihusisha na uchimbaji wa graphite madini muhimu kwa teknolojia ya kisasa kama betri za magari ya umeme, simu janja na vifaa vya kielektroniki. Mradi huu umechangia ajira nyingi, mapato ya Halmashauri na kuinua hali ya maisha ya wananchi wanaozunguka eneo la mgodi.

Vilevile, Mgodi wa Lindi Jumbo unaendelea kuwa nyota inayoangaza katika sekta ya graphite nchini. Mgodi huu unaendeshwa kwa ushirikiano kati ya wawekezaji wa ndani na kampuni za kimataifa, na umeonyesha mafanikio makubwa katika kuongeza uzalishaji wa graphite yenye ubora wa kimataifa. Mafanikio haya yameiweka Ruangwa katika ramani ya dunia kama eneo lenye mchango mkubwa katika sekta ya nishati safi.

Mkuu wa Wilaya ya Ruangwa, Mhe. Hassan Ngoma, amesema kuwa Serikali inaendelea kusimamia kwa karibu shughuli zote za uchimbaji madini ili kuhakikisha zinanufaisha wananchi na taifa kwa ujumla. Akizungumza wakati wa ziara katika mgodi wa Namungo, Mhe. Ngoma amesema:

“Madini haya ni baraka kwa Ruangwa. Tunahakikisha wawekezaji wote wanatekeleza wajibu wao kwa mujibu wa sheria, kulipa kodi stahiki, kulinda mazingira na kushiriki katika miradi ya kijamii. Huu ni wakati wa wananchi kuona matokeo halisi ya rasilimali zao.”

Kwa upande wake, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Ruangwa, Ndugu Frank Fabian Chonya, amesema sekta ya madini imekuwa kichocheo kikubwa cha maendeleo ya wilaya na imeongeza mapato ya ndani kwa kiwango kikubwa. Akifafanua zaidi, amesema

“Kupitia uwekezaji wa migodi kama Namungo na Lindi Jumbo, tumeweza kuboresha huduma za jamii kama elimu, afya na maji. Pia tunawakaribisha wawekezaji wapya kuja kuwekeza kwa kuzingatia taratibu za Serikali. Ruangwa ni ardhi yenye fursa nyingi na amani ya kutosha kwa uwekezaji.”

Mbali na migodi mikubwa, Ruangwa pia ina maeneo ya wachimbaji wadogo wanaochimba madini ya dhahabu, chuma na vito. Serikali kwa kushirikiana na taasisi mbalimbali imekuwa ikiwapatia elimu ya uchimbaji salama na endelevu ili kuhakikisha rasilimali hizi zinatumika kwa manufaa ya wote bila kuharibu mazingira.

Kwa upande wa wananchi, uwepo wa migodi umekuwa neema kubwa. Elida Joashi, mmoja wa wakazi wa Namungo, amesema kuwa maisha ya wananchi yamebadilika kutokana na shughuli za uchimbaji na uwekezaji wa madini. Akizungumza kwa furaha, amesema:

“Zamani tulikuwa tunategemea kilimo pekee, lakini sasa vijana wengi wanafanya kazi kwenye migodi na wengine wameanzisha biashara zinazotokana na shughuli za madini. Hata barabara na huduma za maji zimeboreshwa kwa kiasi kikubwa.”

Aidha, Halmashauri ya Wilaya ya Ruangwa imeweka mikakati ya kuhakikisha shughuli za madini zinachangia katika maendeleo endelevu. Kupitia mpango wa usimamizi wa mazingira na sera za uwajibikaji kwa jamii (CSR), wawekezaji wa sekta ya madini wamekuwa wakichangia katika kuboresha miradi ya kijamii kama ujenzi wa shule, zahanati, visima vya maji na barabara za vijijini.

Ufaulu wa wanafunzi wa se

...Imetoka Pg 05

kondari umeongezeka kwa kasi. Kwa mujibu wa taarifa za mwaka 2024, ufaulu wa mtihani wa kidato cha nne umefikia asilimia 95.6, kutoka asilimia 91 mwaka 2020. Aidha, idadi ya wanafunzi waliochaguliwa kujiunga na kidato cha tano imeongezeka kutoka wanafunzi 748 mwaka 2020 hadi wanafunzi 1037 mwaka 2024, ishara ya ongezeko la ubora wa elimu.

Kwa mujibu wa mmoja wa wazazi wa wanafunzi wa shule ya sekondari Nambawala iliyopo kata ya Namichiga Bw. Joseph Mkana amesema, "Kabla Serikali haijajenga shule mpya watoto wetu walitembea umbali mrefu sana, walikuwa wakirudi nyumbani wamechoka sana na wengine kuchelewa au kukosa kabisa vipindi na kupelekea ufaulu mdogo sana kwa wanafunzi. Ila hali sasa imebadilika baada ya Serikali, kupitia Halmashauri ya Wilaya Ruangwa kujenga shule mpya karibu na makazi ya wananchi jambo ambalo limetatua kero mbalimbali kwa watoto, wazazi na walimu. Hivyo tunamshukuru sana Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan na uongozi wa Halmashauri kwa kuona umuhimu wa elimu kuwa karibu na jamii".

Kwa ujumla, maendeleo ya elimu ya sekondari katika Wilaya ya Ruangwa chini ya uongozi wa Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan ni ushahidi wa utekelezaji



SHULE YA SEKONDARI RUANGWA



SHULE YA SEKONDARI MBEKENYERA



SHULE YA SEKONDARI NAMICHIGA

Limeandaliwa na Kitengo cha Mawasiliano Serikalini
Halmashauri ya Wilaya ya Ruangwa
Barua pepe: ded@ruangwadc.go.tz
Tovuti: www.ruangwadc.go.tz
S.L.P 51, Ruangwa
Fax: +25532933212